

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA ISHIRINI NA SABA

11 MEI, 2018



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA ISHIRINI NA SABA – TAREHE 11 MEI, 2018

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**222. MHESHIMIWA MARTIN ALEXANDER
MTONDA MSUHA (MBINGA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya mapitio ya mipaka ya baadhi ya maeneo ya kiutawala kama vile Mikoa, Wilaya na Majimbo ya uchaguzi kwani baadhi ya mipaka ya maeneo hayo yana muingiliano unaoleta ugumu wa utoaji wa huduma za jamii;

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuligawa Jimbo la Mbinga Vijijini kwa kuzingatia ukubwa wake wa Kata 29.

223. MHESHIMIWA ANATROPIA LWEHIKILA THEONEST (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Jimbo la Segerea ni kati ya Majimbo yaliyosahaulika katika miundombinu ya barabara na kupelekea mitaa mingi kuwa na madimbwi sugu na mafuriko kila mvua inaponyesha. Kadhia hii imepelekea barabara za mitaa kupitika kwa tabu na kupelekea foleni kubwa katika barabara ya Segerea mpaka Barabara ya Mandela kwa kuwa ndio barabara pekee inayotumika na wananchi:-

Je, ni lini Jimbo hili litatengewa bajeti kwa barabara zake za mitaa kwa kiwango cha lami, changarawe na ujenzi wa mifereji.

WIZARA YA MADINI:

224. MHESHIMIWA FRANK GEORGE MWAKAJOKA (TUNDUMA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:- Je, ni kwa nini Serikali haiwapatii Wananchi wa Mji wa Tunduma ruzuku ya asilimia 0.3 kama ilivyo kwa Wananchi wanaoishi katika maeneo yenye kuchimbwa madini.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

225. MHESHIMIWA LIVINGSTONE JOSEPH LUSINDE (MTERA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Je, Serikali ina mpango gani juu ya wanyama waharibifu hususan Tembo ambao wamesambaa ovyo katika Jimbo la Mtera na kufanya uharibifu mkubwa pamoja na kuua watu.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

226. MHESHIMIWA RITTA ENESHER KABATI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:- Mradi wa machinjio ya kisasa wa Ngerewara uliopo katika Manispaa ya Iringa

umekuwa ni wa muda mrefu sana toka umeanza:-

Je, ni lini Serikali italetwa fedha za kutosha ili kumaliza mradi huo.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

227. MHESHIMIWA ZUBERI MOHAMED KUCHAUKA (LIWALE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Liwale ni Wilaya ya zamani hapa nchini lakini hadi leo haina jengo la Mahakama ya Wilaya zaidi ya jengo lililorithiwa toka iliyokuwa Mahakama ya Mwanzo Liwale:-

Je, ni lini Serikali itajenga jengo la Mahakama Liwale sanjari na nyumba za Watumishi.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

228. MHESHIMIWA ORAN MANASE NJEZA (MBEYA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Barabara Kuu ya kwenda nchi jirani ya Zambia imepita katikati ya makazi ya watu na sehemu za biashara hasa

katika Mji Mdogo wa Mbalizi na barabara hiyo inatumiwa na magari ya mizigo ambayo mara nyingi huwa ni chanzo cha ajali:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara mpya ili kuhakikisha ajali zinapungua.

WIZARA YA NISHATI:

229. MHESHIMIWA YAHAYA OMARY MASSARE (MANYONI MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Je, ni lini Vijiji vya Jeje, Kashangu, Idodyandole, Mbugani, Aghondi, Mabondeni, Kitopeni, Ipande, Muhanga, Damwelu, Kitaraba, Kazikazi, Kintanula na Rungwa vitapatiwa umeme katika Mradi wa REA.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
11 MEI, 2018**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**